


KCU  
QUALITY  
COFFEE



*Kagera Cooperative Union*

---

14/03/2023

**TANGAZO LA KUWATAFUTA MAFUNDI KUMALIZIA UJENZI WA UKUMBI WA  
MIKUTANO KATIKA KIWANJA CHA RUMULI – BUKOBA MANISPAA**

Kagera Cooperative Union (1990) Limited imetenga fedha za kumaliza ujenzi wa ukumbi wa mikutano katika kiwanja cha Rumuli. Inahitaji mafundi wabobezi wa kukamilisha kazi katika maeneo yanayohitaji kumaliziwa kama yanavyoonekana hapa chini:-

- i. Kuezeka
- ii. Kufunga ceiling
- iii. Kufunga alcohbond
- iv. Mfumo wa maji safi na maji taka pamoja na maji ya mvua
- v. Mfumo wa umeme, taa na fen
- vi. Mfumo wa camera na computer
- vii. Kupiga plaster na sakafu
- viii. Kuskimu na kupaka rangi
- ix. Uwekaji wa vigae (floor tiles and wall tiles)
- x. Utengenezaji wa madirisha na milango ya aluminium
- xi. Utengenezaji wa milango ya mbao
- xii. Utengenezaji wa mazingira ya nje.

Mradi utatekelezwa kwa njia ya FORCE ACCOUNT. Mafundi wabobezi wenye sifa katika maeneo yaliyotajwa wanatakiwa kuandika maombi na kuyaleta KCU (1990) Ltd Ofisi Kuu na kuyaweka kwenye sanduku la zabuni lililoko mkabala na Ofisi ya Meneja Mkuu. Inashauriwa fundi aombe na kuandikia eneo lile ambalo yeye anaamini ni mbobezi na itafaa kukiwepo na viambatisho kama uthibitisho "**Technical Proposal**". Mwisho wa kuleta maombi ni siku ya Jumatatu tarehe 20/03/2023 saa nne asubuhi na ufunguzi wa bahasha utafanyika siku hiyo mara tu baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha barua kutimia. Waombaji wanaweza kuhudhuria kikao cha ufunguzi.

Maombi yaletwe kwa mkono na juu ya bahasha paandikwe:-

**MAOMBI YA KAZI YA KUMALIZIA UJENZI WA UKUMBI WA MIKUTANO KATIKA  
KIWANJA CHA RUMULI KAZI NO.....(taja namba ya kazi mojawapo  
unayoiomba) kwa anuani ianyoonekana hapo chini:-**

**MENEJA MKUU  
KAGERA CO-OPERATIVE UNION (1990) LIMITED  
S.L.P. 5,  
BUKOBA.**